Zanzibar Broadcasting Corporation

P.O.BOX 314 Zanzibar Tanzania, Phone : 255 2231236
Email: info@zbc.go.tz, Website : www.zbc.go.tz

# TANGAZO

## LA NAFASI ZA KAZI KATIKA SHIRIKA LA UTANGAZAJI



# Utangulizi

Shirika La Utangazaji Zanzibar **(ZBC)** ni Shirika la Umma ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria namba 4 ya mwaka 2013, ZBC ina jukumu la kuhakikisha inawapatia habari, matukio na makala mbali mbali jamii ya Taifa la Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, anuani yake ni S.L.P 314, Karume House - Zanzibar,

Kwa msingi huo, Shirika la Utangazaji (ZBC) linatangaza nafasi za kazi za kada zifuatazo ili kuimarisha utendaji wa kazi zake. Hivyo wote wenye sifa, umri usiozidi miaka 46 ya kuzaliwa ,uwezo na vigezo wanaalikwa kutuma maombi yao ili kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **FUNDI MITAMBO DARAJA LA II**<br>**NGAZI YA MSHAHARA ZPSG-08** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **DAR ES SALAAM** |
| **NAFASI** | **MOJA (1)** |
| MAJUKUMU YA KAZI | • Kusakinisha, kusanidi, na kuendesha vifaa vya utangazaji ikiwa ni pamoja na Transmita, antena, Video & Audio Routers, kamera za video, na mifumo ya kiotomatiki (Automation System).<br>• Kuweka na kusimamia matangazo ya moja kwa moja, kuhakikisha usambazaji wa haraka na ubora wa juu.<br>• Kufanya matengenezo ya kawaida na ukaguzi wa kinga kwenye vifaa vyote vya utangazaji.<br>• Kutambua na kutatua matatizo ya vifaa haraka ili kupunguza muda wa kupungua na kukatizwa kwa matangazo.<br>• Kufuatilia viwango vya utangazaji ili |

| | |
|---|---|
| | kuhakikisha ubora bora na ufuataji wa viwango vya sekta.<br>• Kurekebisha mipangilio ya vifaa ili kusahihisha matatizo ya viwango, sauti na video inapohitajika.<br>• Kutoa msaada wa kiufundi kwa watangazaji, timu za uzalishaji, na wafanyakazi wengine.<br>• Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya matumizi ya vifaa vya utangazaji na programu<br>• Kuhakikisha shughuli zote za utangazaji zinakubaliana na kanuni na viwango vingine vinavyohusika.<br>• Kuhakikisha vifaa vipo katika hali ya usalama na usafi.<br>• Kusimamia utendaji kazi wa mafundi wote waliopo chini yake<br>• Kurikodi kwenye "log book" matengenezo na taarifa zote za matumizi ya mitambo.<br>• Kubuni mbinu mpya za kuimarisha mitambo mipya ya Shirika na mazingira yake<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi. |
| **SIFA NA UZOEFU** | • Awe na elimu ya shahada ya kwanza ya Computer Engineering, Computer Science, Electronics and Telecommunication kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>• Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta<br>• Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea<br>• Awe na umri usiozidi miaka 46<br>• Uzoefu ni sifa ya ziada |

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **FUNDI MITAMBO DARAJA LA II**<br>**NGAZI YA MSHAHARA ZPSG-08** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **PEMBA** |
| **NAFASI** | **MOJA (1)** |
| MAJUKUMU YA KAZI | • Kusakinisha, kusanidi, na kuendesha vifaa vya utangazaji ikiwa ni pamoja na Transmita, antena, Video & Audio Routers, kamera za video, na mifumo ya kiotomatiki (Automation System).<br>• Kuweka na kusimamia matangazo ya moja kwa moja, kuhakikisha usambazaji wa haraka na ubora wa juu.<br>• Kufanya matengenezo ya kawaida na ukaguzi wa kinga kwenye vifaa vyote vya utangazaji.<br>• Kutambua na kutatua matatizo ya vifaa haraka ili kupunguza muda wa kupungua na kukatizwa kwa matangazo.<br><br>• Kufuatilia viwango vya utangazaji ili kuhakikisha ubora bora na ufuataji wa viwango vya sekta.<br>• Kurekebisha mipangilio ya vifaa ili kusahihisha matatizo ya viwango, sauti na video inapohitajika.<br>• Kutoa msaada wa kiufundi kwa watangazaji, timu za uzalishaji, na wafanyakazi wengine.<br>• Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya matumizi ya vifaa vya utangazaji na programu<br>• Kuhakikisha shughuli zote za utangazaji zinakubaliana na kanuni na viwango vingine vinavyohusika.<br>• Kuhakikisha vifaa vipo katika hali ya usalama na usafi.<br>• Kusimamia utendaji kazi wa mafundi wote waliopo chini yake<br>• Kurikodi kwenye “log book” matengenezo na taarifa zote za matumizi ya mitambo.<br>• Kubuni mbinu mpya za kuimarisha mitambo mipya ya Shirika na mazingira yake<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu |

| | |
|---|---|
| | yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi. |
| **SIFA NA UZOEFU** | • Awe na elimu ya shahada ya kwanza ya Computer Engineering, Computer Science, Electronics and Telecommunication kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>• Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta<br>• Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea<br>• Awe na umri usiozidi miaka 46<br>• Uzoefu ni sifa ya ziada |

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **MTANGAZAJI MSAIDIZI DARAJA LA III**<br>**NGAZI YA MSHAHARA ZPSD-01** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **UNGUJA** |
| **NAFASI** | **MBILI (2)** |
| **MAJUKUMU YA KAZI** | • Kusaidia kuandaa na kuandika habari<br>• Kusaidia kutafuta habari za matukio na kuripoti kwa wakati<br>• Kusaidia kutafuta na kubuni mbinu mbali mbali za kukuza na kuendeleza elimu katika fani ya uandishi.<br>• Kusaidia kusoma na kutangaza Habari<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi. |
| **SIFA NA UZOEFU** | • Awe na elimu ya Stahahada katika fani ya Mawasiliano ya umma (Mass Communication) na Uandishi wa Habari (Journalism) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>• Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta<br>• Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea<br>• Awe na umri usiozidi miaka 46<br>• Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada |

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **AFISA SHERIA DARAJA LA 11**<br>**NGAZI YA MSHAHARA -ZPSE-10** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **UNGUJA** |
| **NAFASI** | **MOJA (1)** |
| **MAJUKUMU YA KAZI** | • Kupitia malalamiko ya watumishi wa taasisi yake.<br>• Kutoa ushauri wa kisheria kila unapohitajika.<br>• Kutoa ufafanuzi wa Sheria, Kanuni na miongozo ya kazi.<br>• Kuandaa na kushughulikia nyaraka mbalimbali<br>• Kuandaa na kushughulikia mikataba ya shirika.<br>• Kuhifadhi kumbukumbu na majalada<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na mkuu wake. |
| **SIFA NA UZOEFU** | • Awe na elimu ya Shahada ya Kwanza au stashahada ya juu ya sheria, kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>• Awe na ujuzi katika masula ya shria za mashirika/kampuni/biashara na haki miliki<br>• Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta<br>• Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea<br>• Awe na umri usiozidi miaka 46<br>• Awe na utambulisho wa cheti kutoka skuli ya Sheria (School of law)<br>• Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada |

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **DEREVA DARAJA LA III**<br>**NGAZI YA MSHAHARA ZPSA-09** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **UNGUJA** |
| **NAFASI** | **MBILI (2)** |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | • Kuchunguza na kuikagua gari atakayopangiwa kazi kabla ya kuanza kutumika kila siku ya kazi<br>• Kufanya matengenezo madodo madogo, kama kutia oil, kubadilisha mpira, kuweka maji n.k kuhakikisha kuwa gari haina hitilafu yeyote wakati akiwa yumo kwenye safari ya kazi.<br>• Kujaza "log Book" kabla ya kufanya safari aliyopangiwa na mara baada ya safari kumalizika ahakikishe log book imesainiwa na afisa aliyefanya nae kazi.<br>• Kutoa taarifa kwa mkuu wake wa kazi juu ya haja na kufanyiwa matengenezo gari baada ya kujulikana tatizo la gari ambayo imepata maharibiko.<br>• Kutunza na kuhakikisha kuwa gari iko katika hali ya usafi wakati wote kuwa muadilifu kwa vitu ambavyo vitasahaulika na watumiaji.<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na mkuu wake. |

| | |
|---|---|
| **NAFASI YA KAZI** | **MHANDISI SAUTI MSAIDIZI DARAJA LA III NGAZI YA MSHAHARA -ZPSD-03** |
| **MUAJIRI** | **SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR** |
| **MAHALA** | **UNGUJA** |
| **NAFASI** | **MOJA (1)** |
| **MAJUKUMU YA KAZI** | • Kusakinisha, kusanidi, na kuendesha vifaa vya utangazaji ikiwa ni pamoja na Transmita, antena, Video & Audio Routers, kamera za video, na mifumo ya kiotomatiki (Automation System).<br>• Kuweka na kusimamia matangazo ya moja kwa moja, kuhakikisha usambazaji wa haraka na ubora wa juu.<br>• Kufanya matengenezo ya kawaida na ukaguzi wa kinga kwenye vifaa vyote vya utangazaji.<br>• Kutambua na kutatua matatizo ya vifaa haraka ili kupunguza muda wa kupungua na kukatizwa kwa matangazo.<br>• Kufuatilia viwango vya utangazaji ili kuhakikisha ubora na ufuataji wa viwango vya sekta.<br>• Kurekebisha mipangilio ya vifaa ili kusahihisha matatizo ya viwango, sauti na video inapohitajika.<br>• Kutoa msaada wa kiufundi kwa watangazaji, timu za uzalishaji, na wafanyakazi wengine.<br>• Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya matumizi ya vifaa vya utangazaji na program<br>• Kuhakikisha shughuli zote za utangazaji zinakubaliana na kanuni za na viwango vingine vinavyohusika.<br>• Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na mkuu wake. |
| **SIFA NA UZOEFU** | • Awe na elimu ya Stashahada ya Uhandisi sauti Sound Engineering au fani inayolingana kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>• Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta<br>• Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea<br>• Awe na umri usiozidi miaka 46<br>• Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada |

Maombi yawasilishwe kwa barua pepe kupitia email ifuatayo: -

wwwanajira.go.tz

Mwisho wa kutuma maombi ni Tarehe 23 Julai 2024 muda wa saa za kazi.

**Maombi yaambatanishwe na vitu vifuatavyo: -**

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- Nakala ya Cheti cha Kidato cha nne (Form IV).
- Nakala ya Cheti cha Stashahada au Shahada ya kwanza (kwa mujibu wa nafasi anayoomba).
- Maelezo binafsi ya Muombaji (CV).
- Nakala ya Kitambulisho cha Mzanzibari.

Tangazo hili pia linapatikana kupitia tovuti ya ZBC: **www.zbc.go.tz**